# FADHILA ZA MWEZI WA RAMADHANI

<"xml encoding="UTF-8?>

FADHILA ZA MWEZI WA RAMADHANI

Sifa njema zote Anastahiki Allaah Mola wa viumbe vyote na Swalah na salamu zimfikie Mtume .wetu na kipenzi chetu Muhammad (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) na aali zake watoharifu

Ama kwa hakika katika mwezi wa Ramadhwaan kuna fadhila nyingi ambazo mimi nitazitaja kwa uchache, namuomba Allaah Aniwafiqishe 'asaa yawe na manufaa katika Duniya na .Akhera

MWEZI WA QUR-AAN (1
Kama Alivyosema Allaah Mtukufu:
"Mwezi wa Ramadhwaan ni mwezi ambao imeteremshwa Qur-aan ili iwe uongozi kwa watu na [hoja na upambanuzi (Baina ya haki na batil)" [Qur-aan 2:185

Vilevile kama ilivyopokewa na Ibn 'Abbaas (radhiya Allaahu 'anhu) kuwa makusudiyo yake kwa hakika kuteremshiwa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) Qur-aan mwanzo ni katika mwezi wa Ramadhwaan na vilevile Qur-aan mwanzo wa kuteremka ni usiku wa Laylatul-Qadir .na Laylatul-Qadir iko katika mwezi wa Ramadhwaan

Hivyo basi ni juu yetu kufanya juhudi katika mwezi huu kukithirisha sana kusoma Qur-aan. Walikua Salafus-Swaalih (Wema Waliotangulia) wakikilinda kitabu cha Allaah kwa kukisoma na kuyafanyia kazi yaliyokuwemo kwa mazingatiyo. Pia Tunaambiwa kuwa Sayyidnaa Jibriyl ('Alayhis-Salaam) akimfundisha Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) Qur-aan katika mwezi wa Ramadhwaan, na alikuwa 'Uthmaan bin 'Afaan (Radhiya Allaahu 'anhu) kila siku akisoma Qur-aan yote yaani anakhitimisha mara moja kwa siku, kwa maana, msahafu mzima anausoma kwa siku moja. Na walikuwa baadhi yao katika wema wakisoma Qur-aan yote kwa siku tatu, wengine kwa wiki moja na wengine kwa siku kumi. Walikuwa wakisoma Qur-aan .ndani ya Swalah na nje ya Swalah

Allaah Atuwafiqishe mimi na wewe tuisome Qur-aan na kwa mazingatio khasa katika mwezi .huu tufanye juhudi sana ili tuweze kupata fadhila za mwezi huu mtukufu

MWEZI WA SUBIRA (2

Subira ni katika jambo gumu na halipati ila kwa mtu mchaji Allaah na mnyenyekevu kwa Allaah. Na katika kufunga kunatakiwa subira pale mtu anapojizuilia kutokana na kutokula, kunywa, matamanio na mengineyo. Imekua Swawm ni nusu ya subira na subira malipo yake ni pepo kama alivyosema Allaah Mtukufu:

["Kwa hakika (Allaah) Atawapa wenye kusubiri malipo bila ya hisabu" [Qur-aan 39:10

MILANGO YA MOTO INAFUNGWA, MILANGO YA PEPO INAFUNGULIWA NA (3 MASHETANI WANAFUNGWA

Kama ilivyokuja katika Hadiyth iliyopokelewa na Maimamu wawili:

Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema, "Pindi inapokuja Ramadhwaan inafunguliwa milango ya pepo, na hufungwa milango ya moto, na mashetani wanafungwa kwa [Minyororo." [mesimuliwa na Al-Bukhaariy na Muslim

Kwa hakika utaona katika mwezi huu watu wengi wanajitahidi kujiepusha na maasi, watu wanajaa misikitini kwa kufanya ibada ya mwezi huu hii ni kwa sababu mashetani wamefungwa na shetani juu ya uasi wake lakini anauogopa mwezi wa Ramadhwaan na vitimbi vyake vinakuwa dhaifu ndio mana wengi nyoyo zinabadilika wanaswali na kujitahidi kufanya kheri. Lakini ikimalizika Ramadhwaan tu basi Swalah imekwisha kama vile Allaah yupo Ramadhwaan .tu. Huu ni msiba ndugu zangu Waislamu Allaah Asitujaalie katika hao

LAYLATUL QADR (4

Katika mwezi huu kuna siku ya Laylatul-Qadr siku ambayo ni bora kuliko miezi elfu kama Alivyosema Allaah:

"Huo ni usiku wa hishima ni bora kuliko miezi elfu.
Huteremka Malaika na roho (za viumbe watakatifu) katika (usiku) huo
kwa idhini ya Mola kwa kila jambo.
Ni amani (usiku) huo mpaka mapambazuko ya alfajiri"
[[Qur-aan 97:3-5

Imehisabiwa mtu atakapofanya ibada katika usiku huo mmoja ni kama amefanya ibada sawa na miaka 83 na hii ni katika fadhila kubwa kabisa. Na katika kitabu Muwatwaa, Imamu Maalik .amesema

Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) ameona umri wa ummah za mwanzo ni mrefu, na umri wa ummah wake ni mfupi akapewa usiku wa Laylatul-Qadr uwe ni bora kuliko miezi elfu. [[Muwatwaa, 1/321

Hakuna siku tukufu na kubwa kama siku hii ni wajibu kwetu kuutafuta usiku huu katika kumi la mwisho kufanya ibada ili tupate fadhila hizo. Ninamuomba Allaah atuwezeshe kwa hilo, .Aamiyn

DU'AA NI ZENYE KUKUBALIWA (5

Katika hadiyth iliyopokewa na Imaam Ahmad:

Kutoka kwa Jaabir (Radhwiya Allaahu 'anhu) kwa isnadi iliyo nzuri

Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) Amesema: "Kila Muislam du'aa zake ni zenye kukubaliwa atapomuomba katika mwezi wa Ramadhwaan"

Na imepokewa katika Hadiyth kuwa du'aa ya mwenye kufunga pia ni yenye kukubaliwa. Basi mtu ajipinde katika kumuelekea Allaah kumuomba mambo ya kheri ya dunia na akhera aombe pepo ya Jannaatul Firdaus na alete maombi mengine, Allaah Atayapokea maombi yetu, .AAMIYN

:La mwisho ambalo nitakua nimekamilisha maudhui yangu

MWEZI HUU NI MWEZI WA KUTOA (6

Na alikua Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akizidisha kheri nyingi katika mwezi wa .Ramadhwaan

Imepokewa na At-Tirmidhiy kutoka kwa Anas (Radhiya Allaahu 'anhu) Kasema Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) "Bora ya (wakati wa) kutoa sadaqa ni kutoa katika mwezi wa "Ramadhwaa.n

Na imepokewa na Zayd bin Aslam kutoka kwa babake, amesema nimemsikia 'Umar bin Al-Khattwaab (Radhiya Allaahu 'anhu) anasema, "Ametuamrisha Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) tutoe sadaqa nikatoa mali yangu nikasema leo nimemtangulia Abu Bakr nimekwenda na nusu ya mali, akasema Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) kuniambia, "Umewabakishia nini watu wako?" Nikasema, nusu kama hii, na akaja Abu Bakr na kila mali yake Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akamuuliza, "Umewabakishia nini watu wako? Akasema, nimewabakishia Allaah na Mtume wake. Nikasema huyu Abu Bakr hapitiki na kitu "chochote abadan

Kuonyesha wema waliotangulia walikua wakishindana katika kheri lakini tofauti kubwa katika zama zetu hizi watu wanashindana katika mambo ya kidunia na kujifakharisha nayo.

Tunamuomba Allaah Atuonyeshe mema tuyafuate na mabaya tuyawache na tushindane katika kila kheri ili tuwe ni wenye kufuzu na kupata daraja ya juu ya Pepo.

Aamiyn.

MWISHO